

## Mungu hufanya kazi kupitia watu!

“Mungu anafanyaje kazi katika ulimwengu?” Jibu ni rahisi: kupitia watu ambao wanampenda na kumfuata. Katika. Isaya 61:3, watu hawa wanaitwa “Miti ya Haki” imara, dhabiti na yenye mazao ambayoni “Mapando ya Bwana aliyoyapanda kudhihirisha utukufu wake.” Utukufu wa Bwana ni kila kitu bora alichokiumba, upendo, furaha, baraka na kweli.

Mungu anataka miti hii iwe imara na dhabiti, inayozaa matunda bora. Watu hawa ni imara, wamenawiri na kustawi kwa mtazamo na kiroho na pia huzaa matunda kwa wengine. Hata hivyo tunaweza kuwa miti isiyofaa. Tunaweza kosa kuzaa matunda, kudhoofika kimaadili na pia wabinafsi. Mara nyingi tunakuwa mchanganyiko wa tabia zote.

Zaburi 1 inasema watu waliopandwa kando ya mto wa Roho wa Mungu ni kama “miti iliyopandwa kando ya mito ya maji, inayozaa kwa majira yake na ambayo jani lake halinyauki – chochote wafanyacho watafanikiwa.” Kifungu hiki kinatueleza jinsi watu wanaweza kukua na kufanyika miti mikuu kwa kumheshimu Mungu na kuonyesha utukufu wake katika jamii. Jambo la msingi ni kutambua ya kwamba tunahitaji kupandwa kando ya Roho wa Mungu. Mchanga huu unafaa na kwa kuwa unabubujika uzima unaotokana na maji ya uwepo wa Mungu.

Tunaweza kumkaribia Mungu kwa kudumu katika Biblia na maombi. Tunaposhirikiana na wengine katika safari hii na kuhusika katika kutumikia jamii zetu. Tutakapozingatia haya mambo yote basi, tutatimiza andiko na tutahitimu kuwa miongoni mwa watu wanaofanikiwa katika kila jambo, wanaozaa matunda kwa majira yao na wanaonyesha na kudhihirisha utukufu wa Mungu.

Kumfuata Yesu kunaweza kuonekana jambo la ubinafsi kwa jinsi mtu anaweza kujinufaisha. Huo si ukweli kabisa. Mti wowote ule ungetaka kukua na kufika mawinguni, karibu na aliyeuumba. Sisi pia kama miti hii, tunapomkaribia muumba anatubadilisha na kutugeza kwa mfano na matamano yake. Haya ni kwa utukufu wake. Upendo wa Mungu unapofikia watu na kuwabadilisha kimaisha, kiroho, kimtazamo, kimaadili na kwa matendo. Kwa njia hii tutaona utukufu wa Mungu kupitia kwa watu wanaokaa katika maeneo haya.

### Zingatia!

Unda vikundi vya maisha katika Kijiji chako! Kusanya marafiki wachache kutoka sehemu tofauti katika jamii. Ombeni pamoja, jifunzeni Bibilia na kumwomba Mungu awaonyeshe kile anachotaka katika mtaa wenu.

### Omba:


- 1) Upendo wa Mungu unabadilisha na kuboresha maisha ya watu katika maeneo.
- 2) Mungu atawaonyesha jinsi ya kusimama imara katika imani.
- 3) Walio karibu nasi watahisi wamepandwa katika Roho wa Mungu.



“Watu wasiohudhuria ibada zozote wanajitokeza katika vikundi vya maisha na wanakuja kumfahamu Yesu hapo.

Wanahitaji maombi kwa ajili ya jamaa zao ambao hawamfahamu Yesu”

**- Frenk, Simambwe, Tanzania**



Somo hili limetolewa kwa “Maji, Miti na Mbingu” somo linalopatikana kwa Panda: Mafunzo ya msingi ya Vikundi vya Maisha. Kinachopatikana hapa: [dignityonline.org.uk/publications](https://dignityonline.org.uk/publications)